# FUNZO LA 21

1. Je, tatizo kati ya Abramu na Lutu lilikuwa lipi?
-Lutu na Abramu walikuwa na ng'ombe na kondoo wengi na hawakuwa na sehemu ya malisho ya kutosha.

2. Je, ni kwa nini Lutu alichagua mabondeni?
-Kwa sababu kulikuwa na nyasi ya kutosha kuwalisha ng'ombe na kondoo wake.

3. Je, kwa nini Lutu alifanya uamuzi mbaya kuishi mabondeni?
-Kwa sababu Lutu hakumuuliza Mungu afanye nini.
-Kwa sababu Lutu alikataa kumsikiliza Mungu.

4. Je, nini kitakachofanyika tukikataa kumsikiliza Mungu?
-Tutaenda katika Ziwa la Moto wa Milele.

5. Je, ng'ombe, mbuzi au utajiri mkubwa waweza kutuokoa kutokana na Ziwa la Moto wa Milele?
-La.

6. Je, Mungu aliuona uovu wa watu wa Sodoma na Gomora?
-Ndiyo.

7. Je, twaweza kuficha chochote tunachofikiri kutoka kwa Mungu?
-La.

8. Je, twaweza kuficha chochote tunachosema kutoka kwa Mungu?



-La.

9. Je, twaweza kuficha chochote tunachofanya kutoka kwa Mungu?
-La.

10. Je, Mungu alimwambia nini Abramu baada ya Lutu kuhamia mabondeni?
-Mungu alimuambia Abramu kuwa atampa ardhi ya Kanani.
-Mungu alimwambia Abramu pia kuwa uzao wake utakuwa mwingi kama nyota.
-Mungu alisema kuwa uzao wa Abramu utaishi katika nchi nyingine, na baada ya miaka 400, Mungu atawarejesha Kanaani.

11. Je, jina mpya alilopewa Abramu na Mungu ni lipi?
-Ibrahamu.

12. Je, jina mpya alilopewa Sarai na Mungu ni lipi?
-Sara.

13. Je, kwa nini Mungu alimpa Sarai jina mpya?
-Kwa sababu Sarai angekuwa na uzao mwingi.

14. Ingawaje Sara alikuwa mzee sana na tasa, Mungu aliahidi nini?
-Ya kuwa Sara atakuwa mama wa uzao mwingi.
-Ya kuwa Sara atazaa mwana.

15. Je, Ibrahamu na Sara walikuwa na miaka mingapi?

-Abrahamu alikuwa na miaka 100 na Sara alikuwa na miaka 90.

16. Je, kuna chochote ambacho Mungu hawezi kufanya?
-La.

-Abrahamu na Lutu walitengana kwa sababu hakukuwa na nyasi ya kutosha kulisha mifugo wao wote.

-Je, Ibrahamu alielekea wapi?
-Kwenda milimani.

-Je, Lutu alielekea wapi?
-Kwenda mabondeni.

-Je, miji miwili iliyokuwa mabondeni ni ipi?
-Sodoma na Gomora.

-Je, watu wa Sodoma na Gomora walikuwaje?
-Walikuwa waovu.

-Je, Mungu alijua kuhusu uovu wa watu wa Sodoma na Gomora?
-Ndiyo.

-Je, Mungu alijuaje kuhusu uovu wa watu wa Sodoma na Gomora?
-Mungu anaona kila kitu.

-Hakuna chochote ambacho Mungu hakioni.



-Mungu aliona uovu wote wa watu wa Sodoma na Gomora.

Tusome Mwanzo 18:20-21

20-Bwana akasema, Kwa kuwa kilio cha Sodoma na Gomora kimezidi, na dhambi zao zimeongezeka sana,
21-basi, nitashuka sasa nione kama wanayotenda ni kiasi cha kilio kilichonijia; na kama sivyo, nitajua.

-Mungu alijua kuhusu uovu wa watu wa Sodoma na Gomora kwa muda mrefu.

-Watu wa Sodoma na Gomora walimsahau Mungu, je, Mungu aliwasahau?
-La.

-Watu wa Sodoma na Gomora walimsahau Mungu, je, Mungu alisahau dhambi yao?
-La.

-Je, watu wakimsahau Mungu, Mungu atawasahau?
-La.

-Je, watu wakimsahau Mungu, Mungu atasahau dhambi zao?
-La.

-Mungu hawezi sahau dhambi.
-Mungu lazima aadhibu kila dhambi.

-Je, kwa nini ni lazima Mungu aadhibu kila dhambi?

-Kwa sababu Mungu ni mkamilifu.
-Kwa sababu Mungu aliwaumba watu wakamilifu.
-Kwa sababu kila dhambi inampinga Mungu.

-Je, ni kwa nini Mungu hakuwaadhibu papo hapo watu wa Sodoma na Gomora kwa dhambi zao?

-Kwa sababu Mungu alitaka watubu dhambi zao.
-Kwa sababu Mungu alitaka kuwaokoa.

-Je, wakati wa Nuhu, Mungu alisubiri muda gani ili watu watubu dhambi zao?
-Miaka 120.

-Baada ya watu kutokutubu, Mungu alifanya nini?

-Mungu alituma mafuriko ambayo yaliwaharibu watu wote.

-Mungu husubiri watu watubu dhambi zao.
-Lakini watu wasipotubu, Mungu huwaadhibu.

-Je, ni kwa nini Mungu hawaadhibu watu papo hapo kwa dhambi zao?

-Kwa sababu Mungu anataka watubu dhambi zao.
-Kwa sababu Mungu anataka kuwaokoa.

-Je, Mungu huwatisha watu tu, ila hawaadhibu kwa dhambi zao?
-La.



-Mungu ataadhibu kila dhambi.

-Je, unapofika wakati wa Mungu kuwaadhibu wenye dhambi, kuna yeyote anayeweza kumzuia Mungu?
-La.

-Unapofika wakati wa kuwaadhibu wenye dhambi, hakuna anayeweza kuepuka adhabu ya Mungu.

-Siku moja, Mungu aliwatuma malaika wake wawili Sodoma.

Tusome Mwanzo 19:1-3

1-Basi, wale malaika wawili wakaja Sodoma jioni; na Lutu alikuwa amekaa mlangoni pa Sodoma. Lutu akawaona akaondoka akaenda kuwalaki, akainama kifudifudi.
2-Akasema, Bwana zangu, karibuni nawasihi mwingie nyumbani mwa mtumwa wenu, mkalale, mkanawe miguu yenu, hata asubuhi mwondoke na mapema mkaende zenu. Wakasema, Sivyo, lakini tutakaa uwanjani usiku kucha.
3-Akawasihi sana, nao wakaja, wakaingia nyumbani mwake. Akawafanyia karamu, akawapikia mikate isiyochachwa nao wakala.

-Je, kwa nini Mungu alituma malaika wawili Sodoma?

-Mungu alitaka kumuokoa Lutu na jamii yake.

-Awali, Lutu aliishi karibu na Sodoma.
-Sasa, Lutu alikuwa anaishi ndani ya Sodoma.

-Awali, Lutu aliishi karibu na uovu wa Sodoma.
-Sasa, Lutu alikuwa anaishi ndani ya uovu wa Sodoma.

-Je, unaona kile ambacho dhambi ilikuwa inamfanyia Lutu?
-Dhambi ilikuwa inamvuta Lutu karibu na uovu wake.

-Hiki ndicho dhambi huwafanyia watu wote.

-Dhambi huwavuta watu karibu na uovu wake.

-Kama vile dhambi ilivyomvuta Lutu Sodoma, je, dhambi huwafanyia nini watu wote?

-Dhambi huwavuta watu karibu na uovu wake.

-Je, ni nini kilichowafanyikia malaika walipomtembelea Lutu?

Tusome Mwanzo 19:4-9

4-Hata kabla hawajalala, watu wa mji, wenyeji wa Sodoma, wakaizunguka nyumba, vijana kwa wazee, watu wote waliotoka pande zote.

5-Wakamwita Lutu, wakamwambia, Wako wapi wale watu waliokuja kwako usiku huu? Uwatoe kwetu, tupate kuwajua.

6-Lutu akawatokea mlangoni, akafunga mlango nyuma yake.

7-Akasema, Basi, nawasihi, ndugu zangu, msitende vibaya hivi.

8-Tazama, ninao binti wawili ambao hawajajua mtu



mume, nawasihi nitawatolea kwenu mkawafanyie vilivyo vyema machoni penu, ila watu hawa msiwatende neno, kwa sababu wamekuja chini ya dari yangu.

9-Wakasema Ondoka hapa! Kisha wakanena, Mtu huyu mmoja amekuja kwetu kuketi hali ya ugeni; naye kumbe, anataka kuhukumu! Basi tutakutenda wewe vibaya kuliko hawa. Wakamsonga sana huyo mtu, huyo Lutu, wakakaribia wauvunje mlango.

-Watu wa Sodoma na Gomora walikuwa waovu sana.

-Hao watu walinena uongo mwingi, mwingi sana.
-Hao watu waliwashudia wenzao uongo.

-Hao watu waliwalaani jirani zao.
-Hao watu waliiba vitu vya wenzao.

-Hao watu walilala na wake wa wenzao.
-Hao watu waliuana.

-Hao watu walishiriki ngono waume kwa waume.

-Je, watu wa sasa ni kama watu wa Sodoma na Gomora?
-Ndiyo.

-Je, sisi ni kama watu wa Sodoma na Gomora?
-Ndiyo.

-Je, tunalingana aje na watu wa Sodoma na Gomora?

-Tumenena uongo mwingi, mwingi sana.
-Tumewashuhudia wengine uongo.
-Tumewalaani majirani wetu.

-Tumeiba vitu vya watu wengine.
-Tumelala na wake wa waume wengine.
-Tumewaua wenzetu.

-Je, kisha malaika walifanya nini?

Tusome Mwanzo 19:10-17

10-Lakini wale watu wakanyosha mikono yao, wakamwingiza Lutu kwao nyumbani, wakaufunga mlango.
11-Kisha wakawapiga hao watu walioko mlangoni kwa upofu, wadogo kwa wakubwa, hata wakachoka kwa kuutafuta mlango.
12-Basi wale watu wakamwambia Lutu, Je! Unaye mtu hapa zaidi? Wakwe, wanao, na binti zako, na wote ulio nao katika mji, uwatoe katika mahali hapa;
13-maana tutapaharibu sisi mahali hapa, kwa sababu kilio chake kimezidi mbele za Bwana; naye Bwana ametuleta tupaharibu.
14- Lutu akatoka akasema na wakweze, waliowaposa binti zake, akasema, Ondokeni mtoke katika mahali hapa kwa sababu Bwana atauharibu mji huu. Lakini akawa kama achezaye machoni pa wakweze.
15-Hata alfajiri ndipo malaika wakamhimiza Lutu, wakisema, Ondoka, mtwae mkeo na binti zako wawili waliopo hapa, usipotee katika maovu ya mji huu.



16-Akakawia-kawia; nao wale watu wakamshika mkono, na mkono wa mkewe, na mkono wa binti zake wawili, kwa jinsi Bwana alivyomhurumia, wakamtoa wakamweka nje ya mji.
17-Ikawa walipomtoa nje, mmoja alisema, Jiponye nafsi yako usitazame nyuma, wala usisimame katika hilo bonde po pote; ujiponye mlimani, usije ukapotea.

-Malaika waliwashika mikono Lutu, mkewe na binti zao wawili na kuwaongoza hadi nje ya mji.

-Je, Mungu alimwokoa Lutu kwa sababu alikuwa mzuri?
-La.

-Mungu hakumwokoa Lutu kwa sababu alika mzuri.

-Ingawaje Lutu hakuwa kama watu wa Sodoma, alizaliwa mwenye dhambi.

-Lutu alizaliwa katika dhambi kama watu wote.

-Je, kwa nini Mungu alimwokoa Lutu?

-Kwa sababu Lutu alijua kuwa alimtendea Mungu dhambi.

-Kwa sababu Lutu alijua kuwa dhambi yake ilileta kifo cha milele.

-Kwa sababu Lutu alijua kuwa ni Mungu pekee angeweza kumwokoa.

-Kwa sababu Lutu aliamini kuwa Mungu angemtuma mwokozi amwokoe.

-Mungu huwaokoa wanaomwamini.

-Je, ni nini kilichofanyika baada ya malaika kuwaelekeza Lutu na jamii yake nje ya mji?

Tusome Mwanzo 19:24-25

24-Ndipo Bwana akanyesha juu ya Sodoma na juu ya Gomora kiberiti na moto toka mbinguni kwa Bwana.
25-Akaangusha miji hiyo na Bonde lote, na wote waliokaa katika miji hiyo, na yote yaliyomea katika nchi ile.

-Mungu aliwaharibu kabisa watu wa Sodoma na Gomora.

-Mungu anachukia dhambi yote.
-Mungu anaadhibu dhambi yote.
-Mungu anaadhibu dhambi yote kwa kifo cha milele.

-Nyakati za Nuhu, Mungu aliwaharibu watu wote kwa mafuriko.

-Pale Sodoma na Gomora, Mungu aliwaharibu watu wote kwa moto.

-Malaika walipowachukuwa Lutu, mkewe na binti zao wawili nje ya mji, waliwaambia wasiangalie nyuma.



-Lakini mke wa Lutu hakutii.

Tusome Mwanzo 19:26

26-Lakini mkewe Lutu akatazama nyuma yake, akawa nguzo ya chumvi.

-Mungu alimbadilisha mke wa Lutu akawa nguzo ya chumvi.

-Je, ni kwa nini Mungu alimgeuza mke wa Lutu akawa nguzo ya chumvi?

-Kwa sababu mke wa Lutu hakumtii Mungu, aliangalia nyuma.

-Je, kwa nini mke wa Lutu aliangalia nyuma?

-Kwa sababu alipenda dhambi yake.
-Kwa sababu hakutaka kuwacha dhambi yake.

-Mungu anachukia dhambi.
-Mungu huadhibu dhambi.
-Mungu huadhibu dhambi kwa kifo cha milele.

-Kama utapenda dhambi yako kama mke wa Lutu, Mungu atakuwadhibu kwa kifo.

-Kama hutaki kuwacha dhambi yako kama mke wa Lutu, Mungu atakuwadhibu kwa kifo.